37

# HALMASHAURI YA MJI MDOGO WA MGOLOLO

KIJIJI CHA MAKUNGU,
S. L. P. 22,
MGOLOLO.

17.04.2008.

KUMB. NO. MK/MG/VOL.3/F No.1/2/2008

MKURUGENZI WA
GREEN RESOURCES LTD,
S. L. P. 108,
MAFINGA.

YAH: **KUWASILISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAKUNGU KILICHOFANYIKA TAREHE 16.04.2008 OFISI YA KIJIJI**

Rejea na mada ya hapo juu.

Naomba kuwasilisha muhtasari wa kikao kilichofanyika tarehe 16.04.2008 katika ofisi ya kijiji.
Nyuma ya barua hii nimeambatanisha muhtasari wa kikao hicho.

Natanguliza shukrani.
Ahsante sana

AFISA MTENDAJI WA KIJIJI
KIJIJI CHA MAKUNGU
MGOLOLO_MUFINDI

Ndimi,

E. P. MHELELA
AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA MAKUNGU

**Nakala:**

1. Mhe. Diwani – kata ya Makungu
2. WEO – kata ya Makungu (S. L. P. 116, Mgololo).

**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAKUNGU**
**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA KILICHOFANYIKA TAREHE 16.04.2008**
**KATIKA UKUMBI WA OFISI YA KIJIJI CHA MAKUNGU**

MAHUDHURIO – KIAMBATANISHO KIPO NYUMA YA MUHTASARI

**AGENDA:**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. MAOMBI YA ARDHI KUTOKA GREEN RESOURCES LTD
3. KUFUNGA KIKAO.

**AGENDA NA. 1 – KUFUNGUA KIKAO**

Afisa mtendaji wa kijiji alisimama na kuwashukuru wajumbe kwa mahudhurio mazuri. Baada ya kuwashukuru aliomba wajumbe wajitambulishe, hii ni pamoja na ugeni. Baada ya zoezi la utambulisho Afisa mtendaji alimwomba mwenyekiti afungue kikao.

Mwenyekiti alisimama na kuwashukuru wajumbe kwa kufika kwao kwenye kikao. Aliendelea kusema kuwa leo tuna agenda moja tu ya maombi ya ardhi kwa ajili ya bustani ya miche ya miti kwa kampuni ya Green Resources. Baada ya kusema maneno hayo alisema kikao kimefunguliwa yapata saa 5:30 asubuhi.

**AGENDA NA. 2 – MAOMBI YA ARDHI GREEN RESOURCES LTD**

VEO alisimama na kumwomba mjumbe mmoja asome barua ya maombi. Mjumbe alisimama na kusoma barua ya maombi, barua hiyo imeambatanishwa na muhtasari. Baada ya barua kusomwa mwenyekiti aliwakaribisha waombaji ili watoe maelezo zaidi.

Waombaji walitoa ufafanuzi kuwa maelezo yaliyomo kwenye barua ya maombi tutayatekeleza endapo tutapewa eneo, hata hivyo walisisitiza kuwa; hata yale ambayo hayamo kwenye barua tutayafanya endapo kijiji kitakuwa na uhitaji.

Waliendelea kusema kuwa tunaomba tupewe eneo hili mapema ili tuanze kulifanyia kazi. Pia walituomba tuorodheshe vipaumbele vyetu ambavyo wanaweza kuanzia. Baada ya maelezo ya waombaji mwenyekiti alikaribisha maoni, mapendekezo, maswali mbalimbali kutoka kwa wajumbe wa halmashauri ya kijiji.

Wajumbe walichangia kuwa eneo hilo mwekezaji asipewe moja kwa moja bali aazimwe kwa kipindi fulani. Pia walisema kuwa kuwe na mkataba wa makubaliano. Wajumbe waliendelea kusema kuwa ahadi zilizopo kwenye barua wanaomba zitekelezwe.

Wajumbe walisema kwa kampuni hiyo ni muhimu kuwepo katika kijiji chetu kwani tumeona mafanikio wanayoyapata vijiji ambavyo kampuni hiyo imewekeza kama vile: wananchi kupewa miche ya kupanda na kusaidiwa kujenga shule, zahanati n.k.

**AZIMIO**

Wajumbe walichangia hoja hiyo kwa nyakati tofauti hasa wakizingatia umuhimu wa mwombaji kwa wananchi.

- Wajumbe kwa pamoja walisema kuwa mwekezaji apewe ardhi hiyo kwani wananchi watanufaika kwa kupata ajira na kupewa miche ya kupanda, kusaidiwa miradi mbalimbali kama vile afya, elimu, miundombinu n.k.

KIJIJI ... MGOLOLO

Donatus

Nakala halisi Mwajala Hemed 19-07-2018

AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MAKUNGU S.L.P 22 MGOLOLO

- Mwekezaji apewe ardhi hiyo kwa muda wa miaka 20. Hata hivyo mazungumzo baina ya mwekezaji na serikali ya kijiji yataendelea kuwepo kutegemeana na uhitaji. Hata hivyo muda huo waweza kupunguzwa endapo ahadi na utekelezaji wake hautatekelezeka.

- Wajumbe walipendekeza vipaumbele vya mwekezaji vya kuanzia kama ifuatavyo; hii ni pamoja na ahadi zake.

**Kipaumbele no. 1 – Elimu**
Tunaomba tusaidiwe kujengewa madarasa ya shule ya msingi Mabaoni (block) lenye madarasa matatu katika shule hiyo kwa kuanzia.

**Kipaumbele no. 2 – ofisi bora nay a kisasa inayokwenda na wakati**
Tunaomba tusaidiwe kujengewa ofisi ya kijiji cha Makungu.

**AGENDA NA. 3 – KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti aliwashukuru sana wajumbe kwa michango yao mbalimbali na kuwa wawazi katika kuchangia hoja hii kwa kina. Pia aliwashukuru wawakilishi wa Green Resources Ltd kwa kuleta ombi hili ambalo litaleta manufaa makubwa katika kijiji kama barua yao ilivyojieleza.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 8:15 mchana

M/KITI WA SERIKALI YA KIJIJI
KIJIJI CHA MAKUNGU
MGOLOLO

S. J. Ndenga
Mwenyekiti

AFISA MTENDAJI WA KIJIJI
KIJIJI CHA MAKUNGU
MGOLOLO_MUFINDI

..............................
E. P. Mhelela
Katibu.

Nakala halisi Mwagale Hemed
19.07.2018

M/KITI WA SERIKALI YA KIJIJI
KIJIJI CHA MAKUNGU
MGOLOLO

Donatus Mnoge

AFISA MTENDAJI
KIJIJI CHA MAKUNGU
S.L.P 22 MGOLOLO

HALMASHAURI YA KIJIJI ...
KIKAO CHA HALMASHAURI YA KIJIJI ...
TAREHE 16/4/2008 SAA 4:00 ASUBUHI OFISI YA KIJIJI

| NO | JINA LA MHUSIKA | JINSIA ME | JINSIA KE | CHEO | ATOKAKO MHUSIKA | SAA | SAIN |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | S. J. NDENGA | ✓ | - | M/KITI | MAKUNGU | | [signature] |
| 2 | G. NDONE | ✓ | — | MWEO | MAKUNGU | 0930 | [signature] |
| 3. | R. MFUGALE | — | ✓ | MJUMBE | " | 400 | [signature] |
| 4. | C. SUTTA | ✓ | — | —"— | LUGOLILO | 4:00 | [signature] |
| 5 | E. D. ~~MAHELELA~~ | ✓ | | VEO | MAKUNGU | 4:05 | [signature] |
| 6 | A. KITUNGULU | ✓ | | MJUMBE | MAKUNGU | 4:30 | [signature] |
| 7 | TITO J. KIHZO | ✓ | | FOREST ASST | " | 4:0 | [signature] |
| 08 | Deus K. Mponzi | ✓ | | MJUMBE | MAKUNGU | 430 | [signature] |
| 9 | TUSE | | | | | | |
| 10 | Em BUSEGA GNIVOPA | | ✓ | MJUMBE | MAKUNGU | 4:30 | Busega |
| 11 | Y. N. MKOLA | ✓ | | —"— | MAKUNGU | 4:30 | [signature] |
| 12. | G. MPILUKA | ✓ | | —"— | KIHANDYE | 4:30 | [signature] |
| | | | | —o— | MSIMAMIZI | 4:30 | [signature] |
| 13 | Amon Kivambilo | | | MWINJILISTI LUTH | MAKUNGU | 4:30 | [signature] |
| 14 | DONATUSI MNOGA | ✓ | | MJUMBE | MAKUNGU | 4:30 | [signature] |
| 15 | WAMBURA HAPJOBE | ✓ | | MKARABISHAJI K/WA CCM | KATA MAKUNGU | 4:30 | [signature] |
| 16 | MNYAGILULO U | ✓ | | MJUMBE | MABATINI | | [signature] |
| 17 | P. MVUNG'EMEKE | ✓ | | | MABATINI | 11.00 | [signature] |
| 18. | T. M. Nyalo | ✓ | | Mjumbe | MABATINI | 11.30 | [signature] |
| 19 | J. MHAZALA | ✓ | | WAEO | MAKUNGU | 11.00 | [signature] |
| 20 | B. KALINGA | ✓ | | MHASIBU | MAKUNGU | 11.00 | [signature] |
| 21 | E. MBOGELA | ✓ | | M/M | MAKUNGU | 11 | [signature] |
| 22 | H. MLAWA | ✓ | | MJUMBE | MAKUNGU | 11 | [signature] |
| 23 | ELIZABETI | | ✓ | MCHUNGAJI K.K.K.T. | TOWNSHIP | 11 | [signature] |
| 24 | TITUSI KIMBAVALA | ✓ | | MHUDUMU | MAKUNGU LUC AV | 11 | [signature] |
| 25 | RONES CHAULA | ✓ | ✓ | MKITI KAMATI K/USHARIKA | LOLE Luthera | | Ti Kimbavala |
| 26. | MARIA MLAWA | | ✓ | MJUMBE | MAKUNGU | 11 | [signature] |

[Stamp: SERIKALI YA KIJIJI ... MGOLOLO] [signature]
Donatus Mnoga

Nakala halisi

Mwagala Hemed
19.07.2018

[Stamp: KAIMU MTENDAJI KIJIJI CHA MAKUNGU S.L.P 22 MGOLOLO]